

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO**

*SimuNamba: 027-2552000*  
*Fax Namba : 027-2552020*  
*E-Mail: [ded@kitetodc.go.tz](mailto:ded@kitetodc.go.tz)*  
*[info@kitetodc.go.tz](mailto:info@kitetodc.go.tz)*



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P. 98,  
KITETO,  
MANYARA.

16/02/2022

**TANGAZO LA UKODISHAJI WA VIBANDA VYA STENDI YA MABASI,SOKO  
KUU LA KIBAYA NA UWANJA WA MICHEZO.**

Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto inawatangazia wananchi wote, watu binafsi na Makampuni kuomba Zabuni ya ukodishaji wa vibanda vya Biashara vilivyopo Stendi ya Mabasi,Soko kuu la Kibaya na Uwanja wa Michezo.

**MASHARTI YA ZABUNI YA UKODISHAJI WA VIBANDA**

**Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo kamili na vivuli vya nyaraka zilizothibitishwa na mwanasheria.**

Mwombaji wa Zabuni anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Zabuni kiasi cha Tshs 20,000/= kwenye benki ya NMB -Jina Kiteto District Council Misc Deposit Akaunti na.50101200051 baada ya kupewa Bill na Idara ya Fedha na Biashara ambayo haitarudishwa hata kama mwombaji wa Zabuni hatateuliwa. Mwombaji wa Zabuni atapewa nyaraka za Zabuni na Katibu wa Bodi ya Zabuni siku za kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 alasiri kuanzia tarehe 18/02/2022 hadi tarehe 04/03/2022.

1. Mwombaji wa zabuni anayetarajia kufanya biashara kwenye Kibanda atalazimika kubandika picha yake ya sasa kwenye kiboma kilichopo kwenye kabrasha la zabuni. Mwombaji yeyote atakayeshindwa kufanya hivyo maombi yake hayatafikiriwa kwenye tathimini na atakuwa amejiondoa moja kwa moja
2. Mwombaji atakayeshinda Zabuni ataingia Mkataba wa mwaka mmoja tu na Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto
3. Mwombaji wa Kibanda ndiye atakuwa mpangaji wa kibanda husika.
4. Mwombaji asiwe na deni lolote analodaiwa na Halmashauri ya wilaya.
5. Kodi ya kibanda italipwa kwa awamu ya kipindi cha miezi mitatu mitatu na mpangaji atatakiwa kulipa kodi kabla ya tarehe 25 ya mwezi unaoanza kulipa awamu nyingine.

6. Kodi ya vibanda ni kama ifuatavyo:-

A. STENDI YA MABASI

- Vibanda vya ndani ya stendi-Tshs 40,000/=
- Vibanda vya nje ya stendi -Tshs 30,000/=

B. UWANJA WA MICHEZO

- Upane wa Kaskazini (vibanda Na.58-73)-Tshs 25,000/=
- Upane wa mashariki (Vibanda Na.1-45)-Tshs 30,000/=
- Upane wa kusini(vibanda Na.118-144) - Tshs 30,000/=
- Upane wa Magharibi (Vibanda Na.74-116)- Tshs 40,000/=

C. SOKO KUU LA KIBAYA

- Vibanda Na. 1-84 na 100-123-Tshs 40,000/=
- Upane wa Kaskazini Vibanda Na. 85-99 -25,000/=

7. Mwombaji wa Zabuni atatakiwa kuwa na Leseni hai ya Biashara anayoenda kufanya kwa kutumia kibanda hicho.

8. Mwombaji atakayeshinda Zabuni atapaswa kutunza Jengo na kuweka mazingira kuwa safi wakati wote na kulikabidhi kwa Halmashauri likiwa katika hali nzuri baada ya mkataba kwisha.


- Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo:

KATIBU WA BODI YA ZABUNI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO,  
S.L.P 98,  
KIBAYA -KITETO.

- Juu ya bahasha iliyofungwa vizuri iandikwe NAMBA YA KIBANDA KINACHOOMBWA.

9. Mwisho wa kuleta maombi na kupokea maombi ya Zabuni ni siku ya Ijumaa tarehe 04/03/2022 saa 5:00 asubuhi kwenye ukumbi wa PMU.

- Maombi ya zabuni ambayo yataletwa nje ya muda uliotajwa hayatahughulikiwa



**JOHN JOHN NCHIMBI**  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**KITETO**

**NAKALA:**

1. Mkuu wa Wilaya Kiteto

2. Watendaji wa Kata

3. Mbao zote za Matangazo

4. Tovuti ya Halmashauri

- Wajulisheni Watendaji wa vijiji na wananchi katika Kata zenu

- www.kitetodc.go.tz

**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR**  
**KITETO DISTRICT COUNCIL**